TANGAZO LA SERIKALI NA. 331 la tarehe 5/5/2023

SHERIA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272)

# AMRI

*(Imetoleewa chini ya kifungu cha 29(d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MBEYA (MBEYA WSSA) YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii litajulikana kama Amri ya Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya WSSA) ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2023.

Marekebisho ya bei

2. Bei za maji safi na usafi wa mazingira za Mbeya WSSA zinarekebishwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitakuwa na masharti yafuatayo:

(a) mnamo au kabla ya tarehe 31 Machi 2023, Mbeya WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) miezi mitatu baada ya kuchapishwa kwa Amri ya Bei katika Gazeti la Serikali, Mbeya WSSA itawasilisha ushahidi kwa EWURA kuwa imewajulisha wateja wake na kutoa elimu ya kutosha kwa wadau wake wakiwemo wateja, viongozi wa serikali, viongozi wa vyama vya siasa na wawakilishi wa taasisi za dini kuhusu Amri ya

Bei;

(c) Mbeya WSSA itatekeleza matakwa ya udhibiti kwa kuwasilisha tozo zilizokusanywa kwa wakati;

(d) Mbeya WSSA, itatekeleza miradi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa;

(e) Mbeya WSSA itafanya uhakiki wa kina wa mtandao wa maji taka ili kutathmini hali ya miundombinu na kuwasilisha mpango wa ukarabati ndani ya miezi miwili baada ya kuchapishwa kwa Amri hii;

(f) Mbeya WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama vilivyoanishwa katika Jedwali la Tatu;

(g) Mbeya WSSA, kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo katika Amri ya Bei ; na

(h) Mbeya WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mbeya WSSA ikilinganishwa na mamlaka nyingine za maji safi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake.

Kufutwa kwa Amri T.S. Na. 807 la 2018

4. uta Amri ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (Mbeya WSSA) ya Bei za Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya ya mwaka 2018 inafutwa.

---

MAJEDWALI

---

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

---

*Tangazo la Serikali Na. 331 (linaendelea)*

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Matumizi($m^3$) | Bei ya Sasa | | Bei Zilizoidhinishwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | | 2022/23 | | 2023/24 | | 2024/25 | |
| | | Sh./$m^3$ | Sh./20L | Sh./$m^3$ | Sh./20L | Sh./$m^3$ | Sh./20L | Sh./$m^3$ | Sh./20L |
| Majumbani | 0-10 | 1,100 | 22 | 1,250 | 25 | 1,400 | 28 | 1,560 | 31.2 |
| | >10-20 | 1,100 | 22 | | | | | | |
| | >20 | 1,300 | 26 | | | | | | |
| Taasisi | 0-30 | 1,500 | 30 | 1,720 | 34.4 | 2,000 | 40 | 2,130 | 46.2 |
| | >30 | 1,700 | 34 | | | | | | |
| Biashara | 0-30 | 1,500 | 30 | 1,750 | 35 | 1,820 | 36.4 | 2,130 | 46.2 |
| | >30 | 1,700 | 34 | | | | | | |
| Viwanda | 0-50 | 1,700 | 34 | 1,950 | 39 | 2,100 | 42 | 2,400 | 48 |
| | >50 | 1,900 | 38 | | | | | | |
| Magati | | 1,000 | 20 | 1,000 | 20 | 1,250 | 25 | 1,500 | 30 |
| Boza | | 2,700 | 54 | 2,700 | 54 | 2,700 | 54 | 2,700 | 54 |

Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama ilivyoainishwa kwenye kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | 26,000 | 26,000 | 26,000 |
| Taasisi | | 26,000 | 26,000 | 26,000 |
| Biashara | | 26,000 | 26,000 | 26,000 |
| Viwanda | | 26,000 | 26,000 | 26,000 |

Tozo za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji (Shilingi kwa Marejesho)

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Taasisi | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Biashara | 30,000 | 30,000 | 35,000 | 35,000 |
| Viwanda | 40,000 | 40,000 | 45,000 | 50,000 |

Tozo za Sasa na Zilizoidhinishwa za Huduma ya Majitaka (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2021/22 |
| Majumbani | 385 | 400 | 450 | 500 |
| Taasisi | 500 | 530 | 590 | 650 |
| Biashara | 575 | 600 | 670 | 740 |

*Tangazo la Serikali Na. 331 (linaendelea)*

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2021/22 |
| Viwanda | 700 | 740 | 830 | 920 |

Tozo za Sasa na Zilizoidhinishwa za Huduma ya Majitaka kwa Wateja Wasio na Huduma ya Maji (Shilingi kwa Mwezi)

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2021/22 |
| Majumbani | 20,000 | 21,000 | 22,500 | 23,000 |
| Taasisi | 24,000 | 25,000 | 28,300 | 31,400 |
| Biashara | 36,000 | 37,800 | 42,400 | 47,000 |
| Viwanda | 36,000 | 37,800 | 42,400 | 45,000 |

Tozo za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kumwaga Majitaka kwenye Mabwawa ya Mbeya WSSA (Shilingi Kwa Tripu)

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2021/22 |
| Magari Yote | 50,000 | 17,000 | 17,000 | 17,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 331 (linaendelea)*

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(d) )*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| MAELEZO YA SHUGHULI | KIASI (SHILINGI MILIONI) | | |
|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Kujenga ofisi ya kanda na nyumba za wasimamizi wa mitambo na walinzi | 235 | 133 | 145 |
| Kununua samani za ofisi | 69 | 15 | 10 |
| Kukarabati matekeo 7 ya maji na kujenga upya mengine matano | 55 | 100 | 80 |
| Kufanya ukarabati mkubwa kwenye machujio ya maji 11 | 220 | 5,000 | 20,000 |
| Kununua mabomba na viungio kwa ajili ya ukarabati wa kilometa 6 za mambomba maeneo ya Imeta, Iziwa, Iduda na Ivumwe | 100 | 110 | 115 |
| Kufanya ukarabati mkubwa wa Matangi matatu ya Imeta, Iganzo na Majengo | 10 | 10 | 10 |
| Kununua mabomba na viungio kwa ajili ya ukarabati wa kilometa 30 za mabomba maeneo ya Mabatini, Itende, Majengo, Foresti ya Zamani, Simike, Soko Matola , Iyela na Nzovwe | 500 | 550 | 600 |
| Kufanya ukarabati mkubwa wa kilometa 7.6 za mabomba ya majitaka maeneo ya Matola, Ghana, Uhindini, Ilolo, Mabatini na Sinde na chemba 31. | 400 | 400 | 400 |
| Kununua kompyuta 12 na printa 5 | 30 | 35 | 40 |
| Kununua mfumo wa kompyuta kwa ajili ya mamlaka | 25 | 30 | 35 |
| Kununua vifaa vya ofisi | 15 | 15 | 15 |
| Kununua samani mpya za ofisi kwa ajili ya kubadili zilipo (meza 12, viti 20 na shelfu 7) | 15 | 15 | 15 |
| Kukarabati magari matatu | 40 | 45 | 45 |
| Kukarabati ofisi ya manunuzi na jengo la wateja, na kujenga jengo la wasimamizi wa pampu Nsalaga | 40 | 35 | 35 |
| Kununua na kufunga dira za maji | 933 | 980 | 1023 |
| Kununua vifaa kwa ajili ya kuchakata data (*Purchase Data processing equipment*) | 219 | 113 | 118 |
| Kununua magari na pikipiki mpya | 465 | 236 | 248 |
| JUMLA | 3,371.00 | 7,822.00 | 22,934.00 |

*Tangazo la Serikali Na. 331 (linaendelea)*

---

JEDWALI LA TATU

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(f))*

---

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Maelezo | Kizio | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Maunganisho Mapya ya Majisafi | No. | 5,000 | 5,000 | 5,000 |
| Upotevu wa Maji | % | 28 | 25 | 20 |
| Kiwango cha Kufunga Dira za Maji kwa Wateja | % | 100 | 100 | 100 |
| Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato | % | 97 | 98 | 98 |

Dodoma,
............, 2023

JAMES A. MWAINYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*